

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

KIKAO CHA SABA

12 SEPTEMBER, 2018



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

KIKAO CHA SABA – TAREHE 12 SEPTEMBER, 2018

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**83. MHESHIMIWA IBRAHIM MOHAMEDALI RAZA
(KIEMBE SAMAKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Jiji la Dar es Salaam linakabiliwa na tatizo la ombaomba wengi na katika baadhi ya maeneo wamejenga miundombinu ya kulala:-

Je, ni lini Serikali itachukua hatua ya kuwaondoa ombaomba katika Jiji la Dar es Salaam.

OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):

84. MHESHIMIWA GIMBI DOTTO MASABA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):- Tanzania inakabiliwa na tishio la mabadiliko ya tabianchi linalosababishwa na uchafuzi wa mazingira hasa wa Viwandani:-

Je, Serikali inatoa kauli gani kwa wamiliki wa Viwanda wanaokiuka Sheria za Mazingira.

85. MHESHIMIWA IGNAS ALOYCE MALOCHA (KWELA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):- Upo uharibifu mkubwa wa mazingira katika Ukanda wa Ziwa Rukwa unaotokana na ukataji miti ovyo, wingi wa mifugo na kilimo kisichozingatia utaalumu; shughuli hizi zinahatarisha kukauka kwa Ziwa hilo kwa miaka ijayo:-

Je, Serikali ina mpango gani madhubuti na wa haraka kunusuru Ziwa hilo hasa ikizingatiwa

kuwa imegundulika Gesi ya Helium katika Ziwa hilo.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

**86. MHESHIMIWA HAMIDA MOHAMED
ABDALLAH (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Mgogoro wa ardhi kati ya Mbuga za Wanyama Selous – Kilwa na Wananchi wanaoishi karibu na Mbuga hiyo umezidi kuwa mkubwa kwa sababu mipaka halali haijulikani. Kwa mfano, mwaka 1974 mpaka halali ulikuwa Mto Matandu, mwaka 2010 mpaka huo ulisogezwa kufikia Bwawa la Kihurumila katika Kijiji cha Kikulyungu:-

- (a) Je, Serikali iko tayari kuhakiki eneo hilo ili kuondoa mgogoro mkubwa uliopo kati ya Wanakijiji wa Kihurumila na Mbuga;
- (b) Je, Serikali iko tayari kutatua mgogoro uliopo kati ya Wananchi wa Kilwa na Mbuga.

WIZARA YA KILIMO:

**87. MHESHIMIWA FELISTER ALOYCE BURA
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:- Wananchi wa Kanda ya Kati ni Wakulima wazuri wa zao la Alizeti:-

Je, Serikali haioni ni muda muafaka sasa wa Bodi ya Mazao Mchanganyiko kuanzisha Mfuko mahsusi wa uendelezaji wa zao la Alizeti.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

88. MHESHIMIWA KHATIB SAID HAJI (KONDE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:- Serikali imekuwa ikitangaza kukua kwa hali ya uchumi wa nchi yetu kila mwaka:-

Je, ni vigezo gani sahihi vinavyoainisha ukuaji wa uchumi wa nchi yetu.

WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:

89. MHESHIMIWA ESTER AMOS BULAYA (BUNDA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Kilimo cha umwagiliaji katika Mji wa Bunda kimekuwa kikitengewa fedha kidogo sana kiasi cha kutokidhi mahitaji ya kazi husika:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuiwezesha Ofisi ya Umwagiliaji ya Wilaya ili kufanya kilimo

kuwa cha kisasa, endelevu na chenye kuleta tija kwa Wananchi wa Bunda.

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

90. MHESHIMIWA RIDHIWANI JAKAYA KIKWETE (CHALINZE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Ni Sera ya Serikali kuhakikisha mawasiliano baina ya Watu wake katika maeneo ya nchi yanawezeshwa na kujengwa kikamilifu:-

Je, Serikali imejipangaje kuhusu utekelezaji wa ahadi ya ujenzi wa daraja la Mto Wami.

91. MHESHIMIWA DANIEL EDWARD MTUKA (MANYONI MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Kampuni ya simu ya Vietel (Halotel) imepewa Zabuni ya kusimika minara ya mtandao wa simu katika Jimbo la Manyoni Mashariki. Kasi ya usimikaji minara hiyo ni ndogo; mfano Vijiji vya Heka, Igwamadete, Isimbanguru, Mangoli, Mafulungu na kipande kirefu cha barabara ya Manyoni – Heka – Sanza hakina mawasiliano ya simu kabisa:-

Je, Serikali ina mkakati gani thabiti wa kuibana Kampuni hiyo ili kutekeleza mkataba wake kwa wakati.

92. MHESHIMIWA ENG. RAMO MATALA MAKANI (TUNDURU KASKAZINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa reli ya Kusini (*Southern Circuit*) ya Mtwara – Mbambabay – Mchuchuma – Liganga.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

93. MHESHIMIWA PASCHAL YOHANA HAONGA (MBOZI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:- Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu imeongeza makato kwa wanufaika wa mikopo kutoka 8% - 15% bila kuwashirikisha wadau mbalimbali pamoja na wanufaika wa mikopo:-

- (a) Je, Serikali haioni kwamba imevunja mkataba wa makubaliano kwa kuwa wakopaji walisaini mkataba wa 8% na siyo 15%;

(b) Ongezeko la makato limewaathiri sana wakopaji na kuwafanya kuwa ombaomba na kuishi maisha magumu sana, Je, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu haioni kama litakuwa jambo la busara kusitisha makato hayo ya 15% mara moja ili kunusuru maisha ya Watumishi waliokopa.

94. MHESHIMIWA ABDALLAH DADI CHIKOTA (NANYAMBA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:- Hivi karibuni Serikali ilikusanya vitabu vyenye dosari vilivyosambazwa Shule za Msingi nchini:-

- (a) Je, Serikali imepata hasara kiasi gani kutokana na dosari hiyo;
- (b) Je, ni hatua zipi zimechukuliwa kwa waliosababisha hasara hizo.

95. MHESHIMIWA DKT. STEVEN LEMOMO KIRUSWA (LONGIDO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

- (a) Je, Serikali ina mikakati gani ya kuboresha Elimu ya Awali;
- (b) Kwa kuwa msingi mzuri wa elimu huanza katika Shule za Awali; Je, Serikali haioni kuwa ni jambo la muhimu kuanzisha shule za Awali na kuajiri Walimu waliofuzu kutoa elimu hiyo katika Shule za Vitongoji hasa Vijijini tofauti na ilivyo sasa ambapo Jamii ndiyo inayozianzisha na kuziendesha Shule hizo kwa kutumia Walimu wasio na taaluma.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

96. MHESHIMIWA SILYVESTRY FRANCIS KOKA (KIBAHA MJINI):

- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha bidhaa za nyama nchini pamoja na mazao mengine yatokanayo na Mifugo.

WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

97. MHESHIMIWA DKT. CHRISTINE GABRIEL ISHENGOMA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi,
Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia Wananchi walio kwenye Vijiji vilivyopo kwenye mpango wa matumizi bora ya ardhi kwa kuwarahisishia upatikanaji wa vitabu vya usajili Wilayani.

III. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

*(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima na
Kusomwa Mara ya Tatu)*

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi wa Mwaka 2018 [The Public Private Partnership (Amendment) Bill, 2018].



(Majadiliano yanaendelea)

DODOMA
12 SEPTEMBER, 2018

S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE